BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR

ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI

MKUTANO WA SABA

Kikao cha Kumi – Tarehe 11 Mei, 2022
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua zitasomwa.

I. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2022/2023.

Mwenyekiti wa Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii:

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kilimo, Biashara na Utalii kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa Mwaka 2022/2023.

## II. MASWALI:

### Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

38. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Serikali kupitia Ofisi ya Mufti inastahili pongezi kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa mafunzo ya ndoa kwa jamii.

(a) Je, utaratibu huo ukoje.

(b) Kwa kuwa mafunzo hayo yanatolewa na jinsia ya kiume, Je, hatuoni kuwa tunawanyima fursa jinsia ya kike.

(c) Kwa kuwa kumekuwa na udhalilishaji mkubwa wa wanandoa sambamba na talaka za papo kwa papo. Kwa nini mafunzo hayo yasiwe lazima kwa kila mwanandoa kabla ya kuoa na kuolewa ili kuzinusuru ndoa zao na kupunguza wajane na watoto wanaoishi na mzazi mmoja.

### Wizara ya Afya:

20. MHESHIMIWA MWANAJUMA KASSIM MAKAME (Nafasi za Wanawake) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa hatua iliyofikia ya ujenzi wa vituo vingi vya afya katika maeneo mbali mbali nchini kwa lengo la kuwaondolea usumbufu wa upatikanaji wa huduma za afya na kuondoa kabisa msongamano wa wagonjwa katika hospitali yetu ya Rufaa ya Mnazi mmoja.

Je, Serikali ina mikakati gani itakayowezesha wananchi wazawa kuajiriwa katika hospitali hizo zinazoendelea kujengwa.

47. MHESHIMIWA KOMBO MWINYI SHEHE (Jimbo la Wingwi) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya:

Kwa kuwa Zanzibar kwa kipindi kirefu tumekuwa na uchache wa wataalamu wa kufanyia ukarabati mashine na vifaa tiba vingine kama vile CT Scanner, Ultra Sound, ECG na X-ray, na kwa kuwa zana hizi hununuliwa kwa bei kubwa nje ya nchi kupitia fedha za walipa kodi wa nchi hii na kutofanya kazi kwa muda mrefu huzorotesha afya za watu na uchumi wao.

(a) Je, Serikali ina tathmini ipi ya uwepo wa mahitaji ya wataalamu hao wa Biomedical Engineering ndani ya Zanzibar.

(b) Je, ni lini Serikali itaanzisha fani ya uhandisi wa vifaa tiba ya kibaiolojia (Biomedical Engineering) katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume (KIST) kurahisisha shughuli za uchunguzi wa magonjwa pamoja na tiba.

<u>Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:</u>

5. MHESHIMIWA NASSOR SALIM ALI (Jimbo la Kikwajuni) – Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahili pongezi kwa kufanikisha mashindano ya kombe la Mapinduzi kila mwaka hususan katika maadhimisho ya miaka 58 ya Mapinduzi Matukufu ya Zanzibar ambayo kwa kweli yalifana sana. Hata hivyo wadau wa michezo nchini wameshauri kutanua wigo wa ushiriki wa timu za Afrika Mashariki na Kati katika mashindano hayo.

(a) Je, Serikali kupitia ZFF haioni umuhimu wa kuzialika timu bingwa za Afrika Mashariki na Kati ili kuyapa hadhi ya Kimataifa mashindano hayo.

(b) Je, Serikali haioni haja ya kuvitumia viwanja tofauti vya Unguja na Pemba kwa kuwa mashindano hayo yanapendwa sana Tanzania nzima.

35. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:

Katika siku za karibuni tumekuwa tukishuhudia ukiukwaji wa maadili yetu ya kizanzibari katika lugha, mavazi na uchezaji wa sanaa.

(a) Je, sisi tukiwa ni jamii inayosifika kwa ustaarabu na maadili yetu tunaelekea wapi.

(b) Ni upi mpango wa kuzienzi na kuzilinda sanaa hizi kwa vizazi vijavyo.

(c) Je, Serikali inaziangaliaje nyimbo za kizazi kipya na

vikundi vya ngoma ya kidumbaki, ambazo zinakiuka maadili yetu.

Wizara ya Maji, Nishati na Madini:

16. MHESHIMIWA MARYAM THANI JUMA (Jimbo la Gando) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Maji, Nishati na Madini:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inastahiki pongezi kupitia Mamlaka ya Maji Zanzibar ZAWA kwa kuhakikisha wananchi wanapata maji safi na salama. Hata hivyo katika Mji wa Wete kumekuwa na matatizo ya ukosefu wa maji ya ZAWA mara kwa mara, tatizo ambalo linatokana na miundombinu pamoja na usumbufu wa visima.

(a) Je, Mamlaka ya Maji (ZAWA) ina mpango gani wa kuwaondoshea kabisa wananchi tatizo hilo ambalo linajitokeza mara kwa mara.

(b) Je, Mamlaka ya Maji (ZAWA) imewahi kufanya utafiti wowote na kugundua sababu zinazoleta usumbufu katika miundombinu ya visima hivyo.

Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

43. MHESHIMIWA ZAWADI AMOUR NASSOR (Jimbo la Konde) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Msitu wa Ngezi Vumawimbi ni miongoni mwa misitu ya awali ya kujivunia, kupitia Wizara yako kumekuwa na taratibu mbali mbali za kuhakikisha kuwa msitu huo hautumiwi, unalindwa na kusimamiwa ili kuweza kubaki kwa maslahi yetu na vizazi vijavyo.

(a) Je, ni kwa kiasi gani Wizara yako inawashirikisha wananchi wa maeneo ya msitu huo ili kuweza kuusimamia na kuulinda.

(b) Kwa kuwa kulikuwa na kamati mbali mbai za uhifadhi wa misitu, Je, Wizara inazitambua kamati hizo sambamba na majukumu yao.

(c) Ni mara ngapi Wizara yako ilikaa kujadili changamoto mbali mbali zinazozikabili kamati za uhifadhi wa msitu huo katika juhudi za kuulinda na kuuhifadhi msiku wa Ngezi.

68. MHESHIMIWA MUSSA FOUM MUSSA (Jimbo la Kiwani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar huko nyuma ilikuwa na mkakati wa kilimo cha pilipili hoho, vanilla na hiliki. Lakini kwa kipindi hiki naona kilimo hiki hakijatiliwa nguvu.

(a) Je, suala hili ni kweli.

(b) Je, mpaka sasa Serikali ina mkakati gani wa kilimo hiki.

<u>Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale:</u>

30. MHESHIMIWA SULEIMAN HAROUB SULEIMAN (Jimbo la Kiembesamaki) Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Utalii na Mambo ya Kale:

Je, huoni haja ya kuongeza baadhi ya shughuli katika sehemu zinazotumika kwa ajili ya shughuli za utalii, kuongeza shughuli (Activities) kwa kubuni vitu au shughuli nyengine za kukuza pato la nchi kupitia utalii wa maeneo hayo ikiwemo Jozani, Kisiwa cha Changuu n.k.

## III. HOJA ZA SERIKALI:

<u>Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali:</u>

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Elimu kwa mwaka 2022/2023.

<u>Waziri wa Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo:</u>

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo kwa mwaka 2022/2023.



Zanzibar,
11 Mei, 2022.

(Raya Issa Msellem)
<u>KATIBU WA BARAZA</u>